

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO

Telegram "AFYA", DODOMA
Nambari ya Simu: +255 026 – 2323267
E- Mail Na. ps@afya.go.tz



Mji wa Serikali Mtumba,
Barabara ya Afya,
S.L. P 743,
40478 DODOMA.

TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI

**UCHUNGUZI WA MWENENDO WA MAABARA YA TAIFA YA AFYA YA JAMII
DAR ES SALAAM**

Kufuatia hotuba ya Mhe. Dkt. John Pombe Magufuli Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya tarehe 3 Mei, 2020 wakati akimwapisha Waziri wa Katiba na Sheria, ambapo pia alibainisha changamoto za utendaji wa Maabara ya Taifa ya Afya ya Jamii, Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Mhe. Umy Mwalimu (Mb) amechukua hatua zifuatazo:-

1. Amemwelekeza Katibu Mkuu (Afya) kuwasimamisha kazi mara moja Mkurugenzi wa Maabara ya Taifa ya Afya ya Jamii Dkt. Nyambura Moremi na Bwana Jacob Lusekelo Meneja Udhhibiti wa Ubora ili kupisha uchunguzi.
2. Mhe. Waziri ameunda kamati ya wataalam wabobezi kwa ajili ya kufanya uchunguzi wa mwenendo wa Maabara ya Taifa ya Afya ya Jamii ikiwemo Mfumo mzima wa ukusanyaji na upimaji wa sampuli za COVID-19.

Kamati hiyo itaongozwa na **Prof. Eligius Lyamuya** kutoka Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi Muhimbili (MUHAS) na ina wajumbe wafuatao:

- | | | |
|----|------------------------|--|
| 1. | Prof. Said Aboud | - Chuo Kikuu cha Afya Muhimbili (MUHAS) |
| 2. | Prof. Gabriel Shirima | - Chuo Kikuu cha Nelson Mandela (NMIST) |
| 3. | Prof. Steven Mshana | - Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Bugando (CUHAS) |
| 4. | Prof. Rudovick Kazwala | - Chuo Kikuu cha Kilimo cha Sokoine (SUA) |
| 5. | Dkt. Thomas Marandu | - Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM) |
| 6. | Dkt. Mabula Kasubi | - Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH) |
| 7. | Dkt. Danstan Hipolite | - Mamlaka ya Dawa na Vifaa Tiba (TMDA) |
| 8. | Bi. Viola Msangi | - Mtaalam wa Maabara Mstaafu |
| 9. | Bw. Jaffer Sufi | - Mtaalam wa Maabara Mstaafu |

Kamati hii itanza **kazi mara moja** na itatakiwa kuwasilisha taarifa yao kwa Mheshimiwa Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto kabla ya tarehe 13 Mei, 2020. Sambamba na uchunguzi wa kamati hii, shughuli za upimaji wa sampuli katika maabara hii zinaendelea.

Imetolewa na:

Catherine Sungura

**KAIMU MKUU WA KITENGO CHA MAWASILIANO YA SERIKALI
IDARA KUU - AFYA**

04 Mei, 2020